**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI**

**Kumb. Na. HW/MUF/S.50/19VOL.XI/123** **23/09/2025.**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mufindi anawatangazia Wananchi wa Kata ya Ikongosi wenye sifa na nia ya kufanya kazi (Ajira ya muda) katika Halmashauri ya Wilaya Mufindi kuomba nafasi ya kazi iliyotajwa hapo chini,

## 1.0 MHUDUMU WA USAFI (NAFASI 3)

### 1.1 KAZI NA MAJUKUMU.

i. Kufanya usafi wa nje na ndani ya jengo kila siku.
ii. Kutunza na kuhifadhi vifaa vyote vya usafi.
iii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mwajiri au Mkuu wako wa kazi.

### 1.1.1 SIFA ZA KUAJIRIWA

Awe amehitimu kidato cha nne, Mtiifu na mwaminifu,awe na uwezo wa kufanya kazi bila kusimamiwa na awe mkazi wa kata ya Ikongosi.

### 1.1.2 Malipo

Malipo yatakuwa Tshs.150,000/= kwa mwezi

### 1.2 MASHARTI YA JUMLA

i. Waombaji wawe ni raia wa Tanzania, mwananchi wa kata ya Ikongosi na wenye umri kuanzia miaka 18 usiozidi miaka 35.
ii. Waombaji wote, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi ya kazi kwa mtendaji wa Kijiji.
iii. Waombaji wawe na akaunti ya benki (NMB, CRDB au NBC), kitambulisho cha Taifa (NIDA) au kitambulisho cha Mpiga Kura, namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) wawili wa kuaminika ambao ni wakazi wa kudumu wa Kata ya Ikongosi.
iv. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
v. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **30/09/2025.**

**MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na cheti cha kuzaliwa na cheti cha elimu, aidha maombi ya barua yaletwe kwa:

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi,
S.L.P 223,
MAFINGA.
OFISI KUU ITULAVANU

**Tangazo limetolewa na;**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI
S.L.P. 223, MAFINGA

**MASHAKA S. MFAUME**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI**